THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/1 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 1**

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

Muda: Saa 2 **Jumatatu, 09 Novemba 2015 mchana**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote.**
3. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Scanned by CamScanner

SEHEMU A (Alama 10)
SUNNAH NA HADITHI

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Kitabu cha Hadithi kilichoandikwa na Hazrat Ally ni

A Al-Muwatta B Arrisala C Al-Qataday
D Al-Bayhaq E Al-Waqid.

(ii) Kwa mujibu wa Hadithi ya Mtume (s.a.w), Muislamu wa kweli ni yule ambaye Muislamu mwenzake anayesalimika na maudhi ya

A ulimi wake na vitendo vyake B mkono wake na maneno yake
C vitendo vyake na mkono wake D maneno yake na vitendo vyake
E ulimi wake na mkono wake.

(iii) Utaratibu wa kuondosha uovu katika jamii ulioelezwa katika mafundisho ya Mtume (s.a.w) una daraja tatu. Daraja hizo ni zipi?

A Kwa moyo, kwa ulimi, kwa mkono B Kwa mkono, kwa ulimi, kwa moyo
C Kwa ulimi, kwa mkono, kwa moyo D Kwa mkono, kwa moyo, kwa ulimi
E Kwa ulimi, kwa moyo, kwa mkono

(iv) Yupi kati ya hawa wafuatao **si** miongoni mwa maswahaba wa Mtume (s.a.w) waliohifadhi Hadithi nyingi za Mtume (s.a.w)?

A Imam Bukhari. B Omar Bin Khattab.
C Anas Bin Malik D Bibi Aisha (r.a).
E Abu Said Al-Khudry

(v) Matini ya Hadithi huwa na maneno yanayoelezea yafuatayo **isipokuwa**

A mwenendo wa Mtume (s.a.w) ulio sehemu ya dini
B yaliyofanywa mbele ya Mtume (s.a.w) akayaridhia au akayakataza
C matendo ya Mtume (s.a.w)
D maelezo na maelekezo ya Mtume (s.a.w) juu ya jambo fulani
E sifa za Mtume (s.a.w) kama mwanadamu

(vi) Aina mbili kuu za Hadithi ni

A Mutawatir na Ahad B Maq-bul na Mahdud
C Sahih na Hasan D Nabawiy na Qudusiy
E Sahih na dhaifu

(vii) Msingi wa elimu ya Hadithi unaotumika kumjua msimulizi wa Hadithi aliye mkweli na asiye mkweli unaitwa

A Isnad waljarh B Al-jarh wamatin
C Aljarh wataadil D Taadil waisnad
E Matin waisnad.

(viii) Hadithi ambayo Isnad yake imeshikana tangu mwanzo wa sanad kwa Mtume (s.a.w) au swahaba inaitwa

A Sahih B Nabawiy C Qudusiy
D Hasan E Mutawatir.

Scanned by CamScanner

(ix) Miongoni mwa wanachuoni ambao walifanya kazi kubwa ya ukusanyaji wa Hadithi katika kipindi cha Tabiin ni Imam Suleiman Bin Ash-ath Sajistani aliyejulikana kwa jina maarufu la Imam

A An-Nasaiy B Al-Tirmidh C Ibn Majah
D Abu Daud E Malik bin Anas

(x) Kazi kuu ya Sunnah ni

A kusimulia mwenenendo mzima wa Mtume (s.a.w)
B kuchambua na kufafanua waziwazi Qur'an Tukufu pale palipokuwa na haja ya kufanya hivyo
C kubainisha yale aliyoyaamrisha na aliyoyakataza Mtume (s.a.w)
D kusimulia mwenendo wa maswahaba katika harakati za kusimamisha Uislamu
E kuchambua na kufafanua mambo aliyoyafanya Mtume (s.a.w) katika maisha ya kila siku

.

Scanned by CamScanner

SEHEMU B (Alama 15)
QUR'AN

2. Oanisha aya za Qur'an zilizopo katika **Orodha A** na Sura za Qur'an zilizopo katika **Orodha B**. Andika herufi sahihi pembeni ya namba kutoka orodha A katika kiijitabu chako cha kujibia.

Orodha A		Orodha B	
(i)	"Na ambao wanatoa mali zao kwa kuonesha watu wala hawaamini (aliyoyasema) Mwenyezi Mungu wala siku ya Mwisho". (4:38).	A	Ujumbe wa Qur'an unawahusu watu wote.
(ii)	"Bila shaka mnao mfano mwema kwa mtume wa Allah kwa mwenye kumuogopa Allah na siku ya mwisho" (33:21).	B	Waislamu tujiepushe na tabia ya Bani Israil juu ya kitabu chao.
(iii)	"Na kama mmoja wa washirikina akikuomba umlinde (ili asikilize maneno ya Mwenyezi Mungu) basi mlinde asikie maneno ya Mwenyezi Mungu" (9:6).	C	Suratut Tyn.
(iv)	"Bila shaka tumeshakupa kushinda kuliko dhahiri" (48:1).	D	Mtume (s.a.w) ndio kigezo cha Muislamu.
(v)	"Na hakuwa mwenye kusoma chochote kabla ya hiki wala hakukiandika kwa mkono wake, ingekuwa hivyo wangefanya shaka wale wanaotaka kubatilisha haki" (29:48).	E	Udhaifu wa madai ya Makafiri kuhusu Qur'an.
(vi)	"Hakika sisi ndio tulioteremsha mawaidha haya na hakika sisi ndio tutakayoyalinda." (15:9).	F	Waislamu tusifanye ria katika amali zetu.
(vii)	"Je! Mnaamini baadhi ya kitabu na kukataa baadhi (yake)? Basi hakuna malipo katika nyinyi ila fedheha katika maisha ya dunia na siku ya kiyama watapelekwa katika adhabu kali ……." (2:85).	G	Quran sio zao la Muhammad.
(viii)	"Mmeharamishwa nyamafu na damu na nyama ya Nguruwe… kinyama kilichokufa…., Na kutaka kujua siri kwa kuagua kwa mabao…" (5:3).	H	Nguzo ya tano ya Kiislamu.
(ix)	"Mtu atamkimbia nduguye na mamaye na babaye. Na mkewe na wanawe" (80:34-36).	I	Jamii ya wanadamu itaendelea kuwa masikini.
(x)	"Naapa kwa mchana. Na kwa usiku unapotanda" . (93 :1-2).	J	Pango la Hiraa.
(xi)	"Je ! Mwenyezi Mungu si hakimu muadilifu kuliko mahakimu wote" ? (95 :8).	K	Siku ya malipo.
(xii)	"Na Mwenyezi Mungu amewawajibisha watu wafanye Hija katika nyumba hiyo…" (3:97).	L	Kushushwa Qur'an kwa ujumla.
(xiii)	"Wale wanaokula riba… hali Mwenyezi Mungu ameihalalisha biashara na akaiharamisha riba …" (2:275).	M	Suratu Dhuha.
(xiv)	"… Manabii, Masidiki, Mashahidi na Masalihi (watu wema). Na uzuri ulioje (kwa mtu) watu hao kuwa rafiki (zake)" (4:69).	N	Hudaibiya ni chanzo cha ukombozi wa Makka.
(xv)	Wahyi wa mwanzo kwa Mtume (s.a.w).	O	Makatazo yaliyomo ndani ya Qur'an.
		P	Qur'an ni neno la Allah (s.w).
		Q	Ahadi ya Allah (s.w) ya kuilinda Qur'an.
		R	Mwenyezi Mungu tuongoze katika njia ya wale uliowaneemesha.
		S	Mkataba wa Hudaibiya.
		T	Wote waliodhulumiwa watapata haki zao.

Scanned by CamScanner

SEHEMU C (Alama 15)
TAWHIID

3. Panga sentensi katika vipengele (a), (b) na (c) katika mtiririko wenye kuleta mantiki. **Andika herufi na namba tu** zinazohusika katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) Maana ya dini kwa mtazamo wa kiislamu inafahamika kama ifuatavyo:
- (i) Taratibu au mfumo huo utakuwa ndiyo dini yake.
- (ii) Ama atafuata dini ya Allah au dini ya wanadamu.
- (iii) Kwa mtazamo wa Qur'an dini ni utaratibu (mfumo) wa maisha.
- (iv) Kwa vyovyote katika kuendesha maisha yake, mwanadamu lazima afuate dini.
- (v) Uwe umeundwa na Mwenyezi Mungu au umeundwa na mwanadamu.

(b) Kuwepo kwa dini nyingi duniani imeelezwa katika Qur'an (109:1-6) kama ifuatavyo:
- (i) Nyinyi mna dini yenu nami nina dini yangu.
- (ii) Wala sitaabudu mnachoabudu.
- (iii) Sema "Enyi makafiri, siabudu mnachoabudu".
- (iv) Wala nyinyi hamtaabudu ninayemuabudu.
- (v) Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu.

(c) Kisa cha nabii Adam (a.s) kuhadaiwa na Iblis peponi kimeelezwa katika Qur'an (7: 20-22) kama ifutavyo:
- (i) Na mola wako akawaita (akawaambia), "Je sikukukatazeni mti huu na kukwambieni ya kwamba Shetani ni adui yenu aliye dhahiri".
- (ii) Naye akawaapia (akawaambia): "kwa yakini mimi ni mmoja wa watoao ushauri mzuri kwenu".
- (iii) Na walipouonja mti ule, aibu zao ziliwadhihirikia na wakaingia kujibandika majani ya (miti ya huko) peponi.
- (iv) Basi akawateka (wote wawili) kwa khadaa (yake)
- (v) Basi Shetani aliwatia waswasi ili kuwadhihirishia aibu zao walizofichiwa na akasema "Mola wenu hakukukatazeni mti huu (kwa sababu) msije kuwa Malaika au kuwa miongoni mwa wakaao milele".

Scanned by CamScanner

SEHEMU D (Alama 30)
FIQH

4. Jibu maswali yafuatayo kwa kifupi kwa **kuandika majibu** katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) Taja mambo manne yaliyo wajibu kufanyiwa maiti wa Kiislamu.

(b) Orodhesha faradhi nne za udhu.

(c) Ainisha hadhi na lengo la kuumbwa mwanadamu.

(d) Taja masharti manne ya kutayammamu.

(e) Tofautisha kati ya zakat inayotolewa kwa mazao ya kumwagilia maji shambani na yale yaliyonyeshewa mvua.

(f) Taja mambo manne yanayobatilisha swaumu.

(g) Eleza kwa kifupi jinsi ya kuondoa najisi ndogo na najisi kubwa.

(h) Taja lengo la Faradhi ya swala.

(i) Ainisha vitu viwili ambavyo Muislamu wa kweli anapaswa kuviangalia anapoendesha maisha yake ya kila siku.

(j) Elezea kwa kifupi umuhimu wa Lailatul Qadr.

(k) Tofautisha kati ya neno Ihram na Ilham.

(l) Elezea kwa kifupi kuhusu aina mbili za Hija.

(m) (i) Fafanua umuhimu wa Zakatul-Fitri.

(ii) Bainisha muda unaofaa kutoa zakatul-fitri.

(n) Eleza kwa kifupi jinsi talaka ya Al-Illa inavyotolewa.

(o) Tofautisha kati ya mahari na maharimu.

Scanned by CamScanner

SEHEMU E (Alama 30)
TAREKH

5. Chagua **neno** au **kifungu cha maneno** (i) – (xxx) ili ukamilishe sentensi (a) – (o) **kwa kuandika majibu sahihi tu** katika kijitabu chako cha kujibia. Maneno au vifungu vya maneno vinaweza kutumika zaidi ya mara moja.

(i) Kisiasa
(ii) Nabii Mussa (r.a)
(iii) Mus'ab bin Umeyr
(iv) Udongo
(v) Qur'an
(vi) Asubuhi
(vii) Madina
(viii) 624 A.D
(ix) Suratul Banii Israil
(x) Ukweli
(xi) Aus
(xii) Uhud
(xiii) Ahzaab
(xiv) Matendo
(xv) Khazraj
(xvi) Salman Al-Farsiy
(xvii) Alama za kuwepo Allah (s.w)
(xviii) Adam
(xix) Jioni
(xx) Utume
(xxi) Nabii Haroon (a.s)
(xxii) Jamaa
(xxiii) Dhahiri
(xxiv) Uaminifu
(xxv) Makuraishi
(xxvi) Siri
(xxvii) Kiuchumi
(xxviii) Suraqah
(xxix) Ramadhani 17
(xxx) Hudaibiya

Maswali

(a) _____ alikuwa msaidizi wa _____ wakati wa Firauni.

(b) Kwa mujibu wa Qur'an, asili ya mwanadamu ni _____ bali pia wameenea duniani kupitia kizazi cha _____.

(c) Mwezi wa Ramadhani ni mwezi ulioanza kushushwa _____ na ndio mwezi aliopewa _____ Mtume Mùhammad (s.a.w).

(d) Kabla ya kufaradhishwa swala tano Mtume na Maswahaba wake walikuwa wakisali sala mbili _____ rakaa mbili na _____ rakaa mbili.

(e) Vita vya Badri vilipiganwa _____ mwaka wa 2 A.H sawa na Januari_____.

(f) Katika mwaka wa 6 A.H, Mtume (s.a.w) na Maswahaba wake walitoka _____ na kwenda kufanya Umra lakini walizuiliwa katika kijiji cha _____.

(g) Sababu ya safari ya Mtume (s.a.w) kwenda Isra imebainishwa katika _____ ambayo ni kuoneshwa _____.

(h) Katika miaka mitatu ya mwanzo Mtume (s.a.w) alilingania kwa _____ kisha aliamrishwa kulingania kwa _____.

Scanned by CamScanner

(i) Mambo mawili maarufu yanayoonesha kuwa mitume hawaathiriwi na mazingira katika maisha kabla ya kupewa utume kwa Mtume Muhammad (s.a.w) ni _____ na _____.

(j) _____ ndiye aliyepewa jukumu na _____ la kufuatilia msafara wa Mtume (s.a.w), alipokuwa akihamia Madina.

(k) Baada ya kuwasili Madina, Mtume (s.a.w) aliziunganisha kabila mbili, ambazo ni _____ na_____.

(l) Mtume (s.a.w) alijitenga na _____ zake kutokana na _____ yao.

(m) Swahaba aliyefariki katika vita vya_____ akidhaniwa ni Mtume ni_____.

(n) Makafiri wa Makka walimpinga Mtume (s.a.w) na Utume wake kwa sababu za _____na _____.

(o) Kabla ya vita vya _____ kijana aliyetoa rai ya kuchimbwa mahandaki ni _____.

Scanned by CamScanner